

Washangaa biashara ya hewa chafu

Na Lugano Mbwina

WAHANDISI wa taaluma mbalimbali nchini wamehimizwa kuanza kubuni miradi ya kuuza hewa chafu, ambayo biashara yake inazidi kupanuka katika masoko ya Ulaya na Marekani.

Rai hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Profesa Mark Mwandosya, katika mkutano na wahandisi, ulioitishwa kuwapa mwamko wahandisi kuhusu eneo hilo jipya la uchumi.

Profesa Mwandosya alisema, biashara ya kuuza hewa chafu ina soko kubwa linalopanuka kwa kasi kutoka dola za Marekani 10 bilioni mwaka 2005 hadi dola 30 bilioni mwaka 2006.

Hata hivyo, biashara hiyo ambayo kwa Tanzania imefikia kiwango cha trilioni, inawanufaisha wakazi wa nchi zinazoendelea za India, China, Brazil na kuiacha Afrika yenye mazingira mazuri ya biashara hiyo ikiwa na ushiriki finyu.

"Tunapozungumzia biashara ya hewa chafu, ina maana tunazungumzia biashara kubwa, kwa hiyo ni changamoto kubwa kwetu tukiwa wahandisi kuanza kuzinduka na kuangalia uwezekano wa kutumia ujuzi wetu wa kihandisi kuanzisha miradi ya kuuza hewa chafu," alisema.

Alisema katika biashara hiyo hakuna kitu kikubwa zaidi ya ufundi wa kihandisi, kwa sababu hewa chafu inatokana na shughuli za binadamu katika kilimo, uendeshaji vyombo vya mafuta, uzalishaji vi-

wandani, ujenzi na maeneo mengine yanaendeshwa kwa taaluma ya kihandisi.

Lengo la mkutano huo ni mwanzo wa kuwakutanisha wahandisi wa aina mbalimbali nchini ili kuwafungua macho katika eneo hilo jipya la biashara ambalo lipo chini ya maafikiano ya Itifaki za Kyoto kuhusu Hifadhi ya mazingira, alisema mmoja wa waandaji, Hubert Meena, kutoka CEEST.

Hata hivyo baadhi ya wahandisi walielekea kushangazwa na kuchelewa kuwafikia taarifa kuhusu biashara hiyo huku wengine wakiwa na habari kuwa wakati wahandisi wakazi wakikosa habari hizo wawekezaji wengi kutoka nje tayari wameomba kuwekeza katika eneo hilo hapa nchini.

Mmoja wa wahandisi hao, aliyejitambulisha kwa jina moja la Dk Salewi, alishangaa kwa nini taarifa muhimu za biashara ya hewa chafu zimechelewa mno kuwafikia wadau (wahandisi), jambo ambalo alisema ndiyo kiini cha nchi hii kutokuwa na maendeleo ya kasi.

Juzi nilikuwa Malaysia na Indonesia, nchi hizi ni changa lakini zimeendelea kwa muda mfupi na wananchi wake wanaishi kama wako peponi kwa sababu serikali zinawashirikisha kwa taarifa muhimu wadau wake.

Kati ya miradi zaidi ya 500 ya biashara ya hewa chafu 21 iko barani Afrika, mingi kati ya hiyo ikiwa Afrika Kusini, Misri, Nigeria na mmoja tu wa Mtoni jijini Dar es Salaam ukiwa katika hatua za mwanzo kutoa umeme kutokana na hewa chafu ya methane kutoka uvundo wa taka.

NA MPIGA PICHA WETU



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Profesa Mark Mwandosya (katika) akifungua mkutano wa wahandisi kuhusu miradi ya biashara ya hewa ili kuhifadhi mazingira jijini Dar es Salaam. Wengine ni K.F Manyika (kulia), kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Mtaalam kutoka Taasisi ya Nishati, Mazingira na Maendeleo Tanzania Hubert Meena.